• BW. M. A. BASHIR

...M. A. Bashir, ...mamizi na muanda... wa Ligi ya Changam... ambayo alianza hivi ...uni katika michuano ...tarajiwa kuendelea ... muda wa miezi ... Bw. M. A. Bashir ... ni mwenyekiti wa ... ya Young Cargo ...tayo imetokea ...endwa sana na ...babiki wa Kandanda ... kwa mchezo wao ...dadi. Yeye pia ni ...andishi wa michezo ... Kandanda.

...AMBI ...AMBI

...kupitia kwa gazeti ... rambi kwa niaba ya ... wotw wa Darasa za ... Abdalla Ahmad Bin ... aliyetariki siku ya ... iliyopita tarehe ishirini ... tano Juni. Mungu ... na amlaze pahali ... Peponi. Pokeeni mikono ... tanzia huku tukikuhaki... kwamba msiba huu ni ... Inshalla Mwenyezi ... ndiye mliwaza na ... Kuweni pamoja ... Kadhalika, ... anawapa mkono wa ... vijana wote wa ... hapa Mombasa ... Ramadhani ya mwaka ... walivyokuwa wakihu... kwa wingi katika darasa. ... shikeni kamba ... kwani mshika kamba ... haanguki. Limithli ... Imutana...

Sheikh Nassor akaribisha Ramadhani

WAISLAMU wa mji wa Mombasa pamoja na vitongoji vyake, sasa wana mwaka mzima tokea waanze kusikiliza darasa za Sheikh Nassor Khamis Abdurhman. Ilikuwa ni katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ya mwaka jana, wakati Sheikh Nassor alipojitokeza uwanjani katika mimbari za Msikiti wa Al-Azhar na Msikiti mpya wa Kaloleni.

Kwa vile kwa wakati huo, jamaa wengi walikuwa bado hawajamjua na kumsikia shekh katika darasa zake, walianza taratibu kuvutika kwa sifa walizokuwa wakizipata kwa marafiki zao. Hakumalizika wiki moja ila darasa za shekh Nassor zikijaa watu. Tunakumbuka wasikilizaji walikuwa wakisali Sla za Taraweikh katika misikiti mbali mbali, na wote baasa ya kumaliza sala alikuwa wakimiminikia msikiti wa Kaloleni kwa darasa za usiku.

Baada ya kumalizika kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Sheikh Nassor ndipo alipoanza kuitembelea misikiti yote mashuhuri ya Mombasa kwa mwito wa Maratibu wa misikiti hiyo. Naam, mambo yaliendelea hivyo, sifa zake zikazagaa na pia zikasambaa hadi kufikia Msambweni na Malindi.

Na kwa hivyo, misikiti mingi ambayo iko baina ya miji hiyo, basi Sheikh Nassor ameshaifika kuitolea waadhi. Kwa vile leo hivi Sheikh nassor ameshakuwa maarufu toka hapa Pwani hadi Bara, itakuwa ni rahisi katika Ramadhani ya mwaka huu kufata taratibu za darasa zake.

Sheikh Nassor ambaye ni mzaliwa hapa Pwani, ni mmoja katika ya wanafunzi wa Kiislamu wa Kenya waliopata mafunzo yao huko Saudi Arabia. Baada ya kumalimyaka kumi huko na kufikia kiwango cha shahada aliandika kitabu chake cha kuhitimia shahada yake ambacho kilipasishwa na Vyuo Vikuu vya Kiislamu vya huko Saudi. Sheikh Nassor ingawa nia Mwanazuoni mkubwa, lakini tabia yake ya kuchangamka na watu, imestajamisha makamo ya watu wazima na vijana. Wakati hupenda kuandamana na vijana kwa mazungumzo bila ya kujibaidisha nao. Tafauti na wanazuoni wetu wengine.

Tumebahatika kupata makala ya kwanza ya Sheikh nassor katika gazeti hili, ambayo ameyaandika kwa mausio ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Makala yake yanaendelea kama ifuatavyo:

UTUKUFU wa mwezi wa Ramadhani ulichomoza baada ya kuja uislamu myaka 1400 iliyopita, ikawa mwezi huu ni pamoja na ile myezi mengine mine iliyotajwa katika Quran, nayo ni: Mfunguo pili, Mfunguo nne — ambao ndio mwezi wa kwanza katika kalenda ya Kiislamu na Rajabu. Hii ndiyo myezi mitukufu peke yake kaitka dini yetu ya Kiislamu. Na mwezi wa Ramadhani umeshinda, hii myengine mine kwa sababu ya mambo matatu yaliyo muhimu kabisa. Kwanza katika mwezi wa Ramadhani imeteremka Quran, ambayo mungu ameisifu kuwa ni uongofu kwa bnadamu. Na sifa hii kuwa Quran ni uongofu ina maana kwamba Mwislamu hawezi kufanikiwa katika maisha yake ya kidunia na ya akheri iwapo hakufuata maongozi ya Quran. Na Quran hiyo imebainisha kila kitu chenye manufaa kwa wanadamu wote, na imeeleza wazi yale Mungu ayatakayo na asiyoyataka. kama Quran hiyo imeeleza wazi wazu uongofu ni upi na upotofu ni upi. Kwa ujumla Quran hii imemwongoza binadamu na kumuonyesha njia nzuri katika kila kipembe cha maisha yake. Na yote hayo yamepatikana ndani ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

La pili ni kwamba katika mwezi wa Ramadhani waislamu wamefaradhiwa saumu ambayo ni nguzo tano za Uislamu. Na maana ya saumu au kufunga katika Uislamu, ni kutia (kuazimia) kwa ajili ya mwenyezi Mungu, ya kujizuia kula na kunywana kukurubiana na mkeo kwa matamanio, tangu kutokea Alfajiri ya kweli mpaka kuanguka (kupotea) kwa jua. Manenohaya yana maana kwamba ukila ukinywa ukivuta sigara au ukikutana na mkeo wakati wa mchana, basi fahamu kwamba wewe huna saumuau hukufunga, na itakulazima siku hizo ulizokula mchana uzilipe (uzifunge tena) baada ya Ramadhani kumalizika. Na mtume wetu amesema: Huenda mwenyekufunga asiwe na chochote katikasaumu yake ila njaa na kiu.

Maneno haya yanamaanisha kwmaba, yako mambo mengine pia ambayo yanaweza yakamharibia mtu saumu yake, kwa mfano kusema uongo, uzushi au kusengegenya. Pia amesema mtume (SAW), saumu ni kinga ya moto. Kwa hivyo mwenye kufunga ajizuie na machafu yote. Iwapo mtu atapigwa vita ama au kutukanwa na mengine, na aseme rohoni mwake, mimi nimefunga mara mbili. Saumu ina fadhili kubwa sana kutoka kwa wenyezi Mungu na malipo ya mwenye kufunga, siri yake iko kwa Mwenyezi Mungu.

La tatu ni kuwa katika mwezi wa Ramadhani kuna Laylat-l-kadri, usiku ambao Quran imeteremshwa. Yaani katika Ramadahani kuna usiku mmoja ambao utukufu wake na fadhila zake unazidi myezi alfu moja. Na hii Laylatulkadri iko katika kumi la mwosho la Ramadhani. Na hakuna jambo lenye natija zaidi kuliko kuhuria misikitini na kusikiliza darasa za tafsiri ya Quran. Ratiba ya darasa zetu Ramadhani hii, itakuwa kama ifuatavyo.

Sheikh Abdalla Sleh Farsy, atakuwa na darasa katika Masjidi Noor (Noor) baada ya sala za Adhuhuri kila siku ya Jumamosi na Jumapili. Pia Shiekh Abdalla atakuwa na darasa zake kawaida katika Msikiti wa Shibu kila baada ya sala za Alasiri. Sheikh Nassor, atakuwa na darasa katika Masjidi-l-Azhar (Guraya) baada ya sala za Adhuhuri, kuanza siku ya za Jumatatu hadi Alhamis. Siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili atakuwa na daras huko sehemu za digo, ng'ombeni, Waa, Tiwi Msambweni kama itakavyopangwa. Na wakati wa Usiku takuwa na darasa kila baada ya sala za Taraweikh siku zote hapo Msikiti wa Kaloleni Sheikh Nassor atashika Surat al Israa na Azhar, atashika Surat Al Baqara. Maswali yote ambayo yamefungamana na Ramdhani na saumu, yatajibbiwas Azhar peke yake. Na ni yale maswali tuu yanayofungamana na darasa ndiyo yatakayojibwa. Maswali nje maudhui moja kwa moja yatadharauliwa.

Nawatakia waislamu wote wa Ulimwengu saumu ya kheri na amani. Mola atutakabilie ibade zetu zote.

• SHEIKH NASSOR

MINISTRY OF CULTURE AND SOCIAL SERVICES

KISWAHILI CREATIVE WRITING CONTEST

With the intention of promoting the growth of a body of literature in Kiswahili, the Ministry of Culture and Social Services and the Kenya Kiswahili Association jointly announce a competition in creative writing in Kiswahili. The contest is open to all Kenyans and is expected to include only original unpublished works. These works must strongly reflect aspects of Kenya's cultural heritage.

The competition will have three winning categories: short story, poetry and drama. The short story should have a minimum of five thousand words. The poetry entries can be either **one** long poem of not less than three thousand words, or a **collection** of poems not less than twenty complete pieces. The play should be a fully developed one-act piece and should take about forty-five (45) minutes to perform. All entries will be retained by the Kenya Kiswahili Association. Prices will be awarded for the best three entries in each category. These prices will be presented to the winners during the Kiswahili International Conference, August 30 to September 4, 1981, Nairobi. All entries with correct address and legibly written must reach:

The Kiswahili Creative Writing Contest
Department of Culture
P.O. Box 67374
Nairobi

on or before July 30, 1981. All entries received will be acknowledged.

TUFUNGENI RAMADHANI KWA SALAMA NA AMANI

...MTUKUFU wa Ramadhani umerudi tena. ...shukuru Mwenyezimungu kwa kutuweka hai baadhi ... tukafunga Ramadhani ya Mwaka 1400 was... Kwani wengi tulikuwa nao pamoja nasi ...Ramadhani ya mwaka jana na leo hawapo pamoja nasi, ... amewahitari. Kwa wote waliopita twawaombea ... nemu peponi. Hii ni nafasi pia ya kuishukuru ...Serikali yetu ya KANU, chini ya Uongozi wa Busara wa ...Mheshimiwa Daniel Arap Moi kwa Kuhakikisha kwamba ... huu ambapo Waislamu watakuwa wakifunga, ...vyakula vingi vyapatikana bila ya tabu.

Serikali ina hamu ya kuondolea tabu za wananchi, ... wananchi wenyewe hupenda kuona tabu ikiwapo ... Asili ya kusema hivi ni kwamba, kuna baadhi ... wafanyaji biashara, ambao wao katika myezi kumi ... hawana maendeleo ya kibiashara, na kwa ... chao hukilipa katika wakati Waislamu ...wanapofunga. Yaani sasa utaiona nazi yauzwa kwa shilingi ... badala ya shilingi moja, na mfano wa mengi kama ... Mfanyi baishara huyu huugojea Mwezi wa Ramadhani ili atese waislamu wenzake. Maana hujua ilivyo... mtu amekaa na njaa mchana kuchwa basi hatajali ... atayoabiwa. Kwa kweli anayefanya baishara ya ... hii, hata akija msikitini kusli huja kuwacheza shere ... lakini imani yake kwa nduguze waislamu ina ...

Kuna baadhi ya watu huupokea mwezi wa Ramadhani ... kubwa. Mara tu Ramadhani inapofika utawaona ... kujitatiza maguo katika mwili na pia amebeba ... la tasbihi yuapita mitaani akijionyesha kwa watu. ... yataka watahamu kwamba Mwenyezi Mungu ... "A saumu ly" yaani hii ibadi ya saumu ni yangu ... peke yangu. Yaani hao masanau wa zamani na ... ya urongo ya hapo kake wote hawakuwahi ... ibada hii kwa hivyo kuuteza shere Mwezi wa Ramadhani ni kumteza shere Mwenyezi Mungu. Na pia ni ... ambao utawaona wanaingia katika misikiti ... sala ya Isah, na mara tu Imam akitoa salam, ... mbio kukimbilia barabara ya Kilindini. Huko ... kama SAFA na MARWA. Utaona wasichana wa ... wakijibebenesha mbele ya ndugu zao wavulana ... Mataa nasru Llahir.

... awatakia waislamu wote saumu ya kheri, ... kwa afya na amani.

COASTWEEK KARAMSHI HARJI

SHARP EL-211

Electronic Calculator

Coast Agents:

KARAMSHI HARJI

Box 81777 Tel: 312373

MOMBASA

SWAHILI CROSSWORD NO. 121



JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

KWENDA KULIA:

1. Kwenye miti hakuna ....
5. Kusanya na kuchukua
6. Bakia
8. Hamu ya maji
10. Post Office
11. Basi, tosha
12. Kimbilia, tapia
14. Ama
15. Kiungo cha maneno
16. Starehe
17. Tamko la kukataa
18. Ama
20. Kipige bei

KWENDA CHINI:

1. .... hasumbuki
2. Vimba, weka makuti juu ya paa
3. Kataa
4. Mji wa Tanzania
7. Namna, jinsi
9. Uitengeneze
13. Uzima, maisha
15. Tia makali
19. Ala, jalada.

Mshindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 120

AZIZ RAJABALI, Sanduku la Posta 49142, NAIROBI.

Mshindi aombwa afike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 120 —

KWENDA KULIA:

1. MWAMBAO, 5. KO, 6. OSHA, 7. MFUPA, 8. OMBA, 10. UTU, 11. URU, 12. EA, 15. SWILA, 18. MIA, 19. AMBA.

KWENDA CHINI:

1. MKONOWE, 2. ADHIBU, 3. ARIFU, 4. LO, 5. KIPARA, 9. ATHI, 13. ASI, 14. TAA, 16. WA, 17. LA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Mshindi wa kwanza kila baada ya wiki mbili atapata zawadi ya Sharp EL-211 Electronic Calculator. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na KARAMSHI HARJI, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 15.7.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.